

TAARIFA YA MIRADI ILIYOTEKELEZWA NA GST KWA KIPINDI KINACHOANZIA 2015 HADI 2019

1. UTANGULIZI

Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini (GST) ni taasisi ya utafiti chini ya Wizara ya Madini na ilianzishwa baada ya Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kupitia The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, Na. 7 ya Mwaka 2017. Taasisi hii imetokana na iliyokuwa Wakala wa Jiolojia Tanzania chini ya Wizara ya Nishati na Madini ya kipindi hicho tangu Mwaka 2005. Wakala huu umetokana na Idara kongwe ya Serikali ya Kikoloni ya Mwingereza iliyojulikana kama Idara ya Jiolojia na ilianzishwa rasmi tokea Mwaka 1925. GST ni taasisi yenye uzoefu mkubwa katika masuala ya utafiti wa madini (*mineral explorations*) na uratibu wa majanga asili ya jiolojia Afrika Mashaiki na Kati.

2. MIRADI ILIYOTEKELEZWA NA GST KWA KIPINDI KINACHOANZIA 2015 HADI 2019

Katika kipindi husika GST ilitekeleza miradi mbalimbali iliyofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande mmoja na kwa upande mwingine Miradi iliyofadhiliwa kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo. Katika kipindi hiki Serikali kupitia GST ilifanya yafuatayo:-

- i Ugani wa jiolojia na jiokemia katika QDS sita (49, 264, 265, 202) katika wilaya za Maswa, Ulanga, Mahenge, kisarawe, morogoro vijijini, Mlandizi ulikamilika. Tafiti hizi zilipelekea kupatikana kwa taarifa za jiosayansi mpya ambazo ni muhimu katika kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini.
- ii Katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kusaidia wachimbaji wadogo, Wizara kwa kutumia Taasisi zake za GST na STAMICO walikamilisha utafiti wa kina wa jiosayansi chini ya mradi wa Usimamizi Endelevu wa Raslimali Madini (SMMRP). utafiti wa kina wa jiosayansi ilihusisha jiolojia, jiokemia na jiofizikia (picha Na.1) ulifanyika kwa lengo la kubaini uwepo na kiasi cha madini kinachopatikana katika maeneo sita ya wachimbaji wadogo ambayo ni Kapanda, D-Reef na Ibindi (Mpanda); Buhemba (Musoma); Katente, Kerezia na Ng'anzo (Bukombe); Itumbi, Mapogolo na Sangambi (Chunya); Kyerwa (Bukoba); na Kiomoni, Mkulumuzi na Kange (Tanga). Matokeo ya utafiti huu yamekadiriwa kuwepo kwa jumla ya wakia **114,464.65 za dhahabu** kwa maeneo ya Katente, Buhemba (Rwabasi), Mpanda (D-Reef and Kapanda) na Itumbi; **tani 403,056,469 za limestone zenye ubora wa 48%** katika maeneo ya Kiomoni na Mukurumuzi (Tanga) na jumla ya **tani 1,409,742.15 za bati**. Matokeo ya utafiti huu yatawasaidia wachimbaji wadogo kuchimba kwa uhakika na hivyo kuongeza mapato yao na pato la Taifa kwa ujumla.



Picha Na.1: Utafiti wa kina –kuchimba Mitaro (*Trenches*) - kutafuta mwelekeo wa *vein* katika eneo la Itumbi




Picha Na. 2: Uchorongaji kwa njia ya RC – Katente



Picha Na. 3: Uchorongaji kwa njia ya DD – Mpanda

- a) Kuboreshwa kwa mfumo wa usambazaji wa taarifa/takwimu za jiosayansi kwa kuanzisha mfumo wa usambazaji wa taarifa za jiosayansi na madini (*Geological and Mineral Information System-GMIS*) pamoja na web portal. Uanzishwaji wa mfumo hii umerahisisha kwa kiasi kikubwa upatikanaji na usambazaji wa taarifa hizi kwa wadau
- b) Kuboreshwa kwa vitendea kazi na miundombinu kupitia mradi wa SMMRP, serikali iliipatia GST vifaa vya kisasa vya maabara na vya ugani. Baadhi ya vifaa vilivyounuliwa ni pamoja na ICP, XRF, AAS with graphite furnace. Upatikanaji wa vifaa hivi umeimarisha utoaji wa huduma za maabara na utendaji kazi kwa ujumla.




Picha Na. 4: Vifaa/machine mpya za uchunguzi zilizonunuliwa kwa ajili ya kuboresha huduma zitolewazo na Maabara ya GST

3. KUFANYA UTAFITI WA JIOSAYANSI KWA KUSHIRIKIANA NA WASHIRIKA WA MAENDELEO


- i. Ramani za jiokemia za nchi nzima (*Country Wide Multi-Element Geochemical Maps*) zinazoainisha wingi wa madini ya aina mbalimbali za metali (k.m. dhahabu, shaba, chuma, nikeli, bati n.k.) katika sehemu mbalimbali za nchi zimetengenezwa (**Ramani Na. 1**). Kazi hii imefanywa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ambao ni *Geological Survey* ya Finland na Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA)

Ramani Na. 1: Ramani inayoonesha uwingi wa madini ya shaba




- ii. Ramani inayoonesha viwango vya ubora wa PH (p^H values) kwenye udongo nchi nzima imechorwa/imetengenezwa. Ramani hiyo inaonesha maeneo yenye PH ndogo na kubwa ambayo ni mikoa ya Mbeya, Njombe, Dodoma-Singida, Manyara, Arusha, Shinyanga na Kigoma. Kutokana na hali hiyo GST kwa kushirikiana na Geological Survey ya Finland (GTK) inaandaa programu ya utafiti wa namna ya kurekebisha PH kwa kutumia miamba. Hivyo GST na GTK itafanya utafiti wa madini yanayofaa kurekebisha udongo ulioathirika (*High acidic and high alkalinity*) kwa lengo la kuboresha udongo ili kuongeza uzalishaji wa mazao kwa maeneo tajwa. **(Ramani Na.2: Ramani inayoonesha viwango vya PH)**

Ramani Na.2: Ramani inayoonesha viwango vya PH



- iii.** Kufanyika na kukamilika kwa utafiti wa jio-sayansi (jiolojia, jiochemia na jiofizikia) katika mikoa ya Lindi na Mtwara ambapo ramani na taarifa za kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini eneo la Nachingwea-Masasi (*Mineral investment promotion map of Nachingwea – Masasi Block*) zimekamilika.

Ramani Na.2: Ramani ya Jiolojia ya Nachingwea-Masasi block.



iii Serikali kupitia GST kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia ya China ilikamilisha utafiti wa jiokemia katika skeli kubwa katika mkoa wa Mbeya na skeli ndogo katika eneo lote la nchi (*Geochemical Mapping for High and Low Density using stream sediment*). Aidha, kupitia mashirikiano haya Atlas ya Jiokemia ya nchi nzima ilichapishwa. Utafiti huu utaleta manufaa kwa taifa hasa katika kujua aina za madini yaliyopo, aina za madini zilizopo kwenye udongo kwa ajili ya kilimo, mazingira na mipango miji.



Picha Na. 5: Waziri wa Madini Mhe. Doto Biteko akionesha Taarifa ya Utafiti wa Jiokemia iliyofanywa katika Mkoa wa Mbeya. Kulia ni Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Jiolojia ya China, Profesa Sun Xiaoming na kushoto ni Kaimu Katibu Mkuu Mathias Abisai.

iv Serikali kupitia GST na kwa mashirikiano na Serikali ya Jamhuri ya Korea kupitia *National Geographic Information Institute (NGII)* ilikamilisha tafiti zifuatazo:-

- a) Utafiti wa jiosayansi katika sehemu za maeneo ya Namtumbo, Momba na Tunduru katika QDS 257, 312, 313, 319 na 320; na
- b) Utafiti wa jiofizikia kwa kutumia ndege katika QDS 312, 313 ulikamilika.



Picha Na. 6: Wataamu wa kutoka GST na Korea wakijadili jambo katika uwanja wa ndege wa Songea kabla ya ndege kupaa kwa ajili ya kufanya utafiti wa jiofizikia